# NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO - MASWALA YA JAMII

**Kipindi cha Nane-"Haki yangu Kuchagua"**

**Mwandishi** : Chrispin Mwakideu

**Redakshoni**: Andrea Schmidt

**Wahusika**:
Eveline(19),Ronnie(14),Betty(12),Mapito(40),mtangazaji, mwanahabari(27) r

## Msimulizi

Hujambo msikilizaji na karibu katika kipindi hiki cha Noa Bongo jenga Maisha Yako tujifunze maswala ya jamii na jinsi ya kushiriki katika siasa. Katika kipindi kilichopita tuliona jinsi Beti na kikundi chake walivyoibuka washindi katika tamasha la uimbaji na Roni na timu yake kuambulia patupu katika kindumbwendumbwe cha fainali ya mchezo wa kandanda. Eveline naye yuko katika njia panda pamoja na kamati yake ya kumpigia debe baada ya kupokea habari kwamba babake amepigwa risasi. Je lilikuwa tukio la uhalifu wa kawaida au ni aina fulani ya kitisho dhidi ya kampeni yake? Sikiliza ukweli huku wakaazi wa eneo la Milimani leo wakipiga kura kumchagua diwani wao katika mchezo kwa jina ´´Haki yangu ya Kuchagua´´

**Onyehso la kwanza: chumba cha kuishi**

**SFX: Sauti ya vyombo vikioshwa…maji**

**1.BETI:** (**akikaribia kulia**) Siamini!

**2.RONNIE**: Hata mimi siamini.. ni nani angelimfanyia hila baba yetu ambaye wakati wote analinda usalama wa kila mmoja..

**3.EVELINE**: Roni usizungumze kana kwamba tayari baba ameshakata roho.. kwa kuwa yeye ni askari basi ni kawaida kupitia haya.. tusubiri.. madaktari wamesema wanaweza kuitoa risasi hiyo mwilini .. ni vigumu kujua kitakachotokea…

**4.BETI**: Siwezi kustahamili.. nikimaliza kuosha vyombo nitakwenda hospitali kumuona baba…namkosa sana (**akilia**)

**5.EVELINE:** Huwezi! Hawaruhusu mtu kumuona akiwa chumba cha wagonjwa mahututi.. subirini afanyiwe upasuaji halafu tutakwenda soteni…

**6.RONNIE**: Na je kuhusu uchaguzi? Bila shaka hutacha kugombea udiwani kwa kuwa baba amepigwa risasi .. ama?

**7.EVELINE**: Niache? Mimi? Kwa kweli tukio hili limenipa moyo zaidi.. sasa nitawaeleza vizuri watu wangu kuhusu ufisadi, ugavi wa rasilimali usio sawa, na uhaini mwengine ambao kila siku unaowakumba watu wangu.

**8.BETI**: Itakuwaje na nje hakutokeki tangu mapaparazi wasikie baba kapigwa risasi?

**9.EVELINE**: Nawaomba radhi kwa hilo.. ni lazima muanze kuzowea maisha ya aina hii .. Roni hebu tazama kama bado wangalipo hapo nje.. watazame kupitia dirishani…

**SFX: Pazia zafunguliwa zikifuatiwa na sauti za kamera zikipiga flashi**

**10.RONNIE**: Aaah! Hizi taa za kamera zinapofusha!!!

**SFX: anafunga pazia**
Inaonekana kuna idadi ya kamera imeongezeka zaidi kuliko jana usiku..kwani hawachoki hawa watu?

**11.EVELINE**: Hiyo ndio kazi yao.. tunachopitia wakati huu ni habari muhimu sana kwao…hata hivyo hatutaketi humu ndani daima… itatubidi tuelekee kituoni kupiga kura … muhimu ni kunyamza kimya…wakitaka kujibiwa niwachieni mimi…

**12.BETI**: Natamani ningelikuwa naweza kupiga kura.. ningelikupigia mara mia moja..

**13.EVELINE:** (akicheka) Mtu huruhusiwa kupiga kura mara moja tu.. tena ni lazima uwe na kitambulisho na kadi ya upigaji kura kwa hivyo ni lazima uwe na miaka kumi na nane au zaidi…

**14.RONNIE**: Sielewi! Kwa hivyo hata kama ninataka kukuchaguwa leo ni lazima nifike miaka kumi na nane? Nataka kukupigia kura lakini siruhusiwi…Hio si haki..

**16.BETTY**: Ulipoteza haki yako pale uliposhindwa kwenye mechi ya fainali…**(akimkejeli Roni)**

**17.RONNIE**: Sipendelei mzaha sampuli hiyo Beti…

**18.EVELINE**: Eeeh nyie acheni kuudhiana.. Wee Roni acha pupa.. bado miaka minne tu kisha utaweza kumchagua umtakaye.. raisi, mbunge na hata diwani ..…

**19.BETI**: Wewe ndio chaguo langu .. kwa hao wote uliowataja…

**20.EVELINE**: Najua nyote ni wendani wangu.. ijapo kura yako nitaisubiri sana.. jamani hebu tuharakisheni nikapige kura…

**SFX: Mlango unafunguliwa na unafungwa**

**<u>Onyesho lapili: kituo cha kupigia kura</u>**

**1.MSIMULIZI:** Siku ya kura ikawadia.. Watu wengi wa kila tabaka na umri walijitokeza kupiga kura.. idadi ambayo haijawahi kuonekana katika historia ya mji huo. .Eveline tayari ametumbukiza kura yake. Sasa, yeye na ndugu zake, Betty na Roni, wamo njiani kuelekea hospitalini.

**2.RONNIE**: Mbona leo kimya hivi? Ziko wapi kelele za siasa? Sisikii ngoma, tarumbeta wala firimbi zikilia kama wakati wa kampeni…

**3.EVELINE**: Hairuhusiwi kufanya kampeni siku ya uchaguzi… Kundi lolote la wafuasi likifanya hivyo mgombeaji wao anaweza kutolewa uchaguzini..

**4.BETI**: Uchaguzini? Mbona sielewi?

**5.EVELINE:** Huo ni ule utaratibu wa kuchagua umtakaye.. na inamaanisha mgombeaji anaweza kukataliwa…

**6.BETI**:Tutajuwa lini kama umeshinda?

**7.EVELINE**: Beti, Usiwe na hakika hivyo kwamba nitashinda.. ninamenyana na wanasiasa wakongwe na hawataniachia kiti hiki kirahisi.. Majibu yanatolewa kabla siku kumalizika lakini sina uhakika kwani inategemea na idadi ya wapiga kura..

**8.RONNIE**: Na je utakaposhinda na wakufanyie mizengwe itakuwaje? Watakapopoteza kura zako na kujaliza za wengine utafanyaje? Unajuwa ni heri mpirani bao likiingia kila mtu

anashuhudia…

**9.BETI**: Ama kama bao halikufungwa.. kama kwenye mechi yenu ya fainali? (**mzaha**)

**10.RONNIE**: (**akasirika**) Betty..una bahati hatuko nyumbani.. ningekutia ngoto..

**11.EVELINE**: Tunapopiga kura tunapenda kuamini uchaguzi umefanyika kwa uhuru na haki. Lakini si hivyo kila mara…Kuna mambo mengi ambayo yamewekwa kuzuia aina yoyote ya udanganyifu.

**12.RONNIE**: Ahh kweli? Kama nini? Una wapelelezi? (**akivutiwa**)

**13.EVELINE:** Karibu na hiyo… lakini katika uchaguzi wanaitwa waangalizi..wao hutoka kila pembe ya dunia kwa zoezi hilo maalum la upigaji kura..hutazama kama matokeo yanawiana na mapenzi ya wapiga kura..pia wapo askari na maafisa wa tume kufanikisha zoezi hilo…

**14.BETI**: Eve..Eve..wadaku wanakuja?

**15.EVELINE**: Nani? Ah unamaanisha waandishi wa habari.

**16.MWANAHABARI**: Hujambo Eveline, naomba dakika moja yako…?

**17.EVELINE**: Wacha dakika, hata nukta pia hupati. Nilikueleza ukweli badala yake ukageuza hadithi yote ilivyokuwa..ukaniharibia sifa na jina..jamii imewapa imani kuripoti ukweli lakini badala yake munasambaza uongo…

**18.MWANAHABARI**: (**aibu**) Pole.. na mpe pole babako pia..namtakia heri ya uponyaji na wewe nakutakia uchaguzi mwema..

**19.EVELINE**: Kwa hiyo sasa unanitakia vyema sio..mimi nikishindwa katika uchaguzi itakuwa ni kwa sababu ya watu kama nyinyi na wale walioharibu mabango yangu. Ingelikuwa waandishi wote ni vibaraka vya wanasiasa na mabwanyenye ingelikuwaje? Nashukuru wapo walio wakweli…hebu twendeni tukamtembelee baba…

**20.MSIMULIZI**: Maneno haya ya Eveline yalimgusa sana mwanahabari huyo, na akaaibika kutokana na uhaini wake. Aliyeyuka mahali pale.. Na huuku kura zikiendelea kupigwa kwa amani, madaktari walifanya bidii kuitoa risasi mwilini mwa Mapito. Eveline, Betty, Roni na baadhi ya wafuasi wakisubiri kwa hamu matokeo ya upasuaji, matokeo hatimaye yanatangazwa redioni…

**Onyesho la Tatu: Hospitali…..Muzik unasikika…**

**1.BETI:** Majibu ya baba yamekawia mno..……

**2.MTANGAZAJI**: (**Muziki unafifia**) Wasikilizaji tumepokea matokeo ya uchaguzi kutoka Milimani..

**3.EVELINE**: (**wahaka**) Shhhhhh! Subiri kidogo Betty…tusikilize matokeo….

**4.MTANGAZAJI**: Haya ndiyo matokeo ya uchaguzi wa Milimani. Mshindi ambaye amepata kura 12,803, idadi kubwa kabisa ya kura iliyowahi kushindwa na mgombea ni….Eveline Mapito! (**tangazo lafifia chini ya sauti ya Betty**). Wa pili ni Ibrahim Mulongo na kura 10,405 na wa tatu ni Samuel Dubu… na

kura 678..

**5.BETTY**: Yeeeeeeee!!!! Ndioooo! Eve! Eve umeshinda! Sasa wewe ni diwani wetu!

**6.RONNIE**: (**akishangilia**) Pongezi dada!

**7.EVELINE**: Asanteni lakini tupungezeni kelele tuko hospitalini.. Natamani kama baba angekuwa mzima wa afya kusikia habari hizi pamoja na sisi.. Ahh…afadhali hatimaye daktari anakuja…

**SFX: Mlango mkubwa unajifungua na kujifunga**

**8.BETI**: Mbona sura yake ina huzuni? (**hofu**)

**9.RONNIE**: Beti, siku zote wewe ni mtaka maovu…

**10.EVELINE:** Subirini.. Tazameni baba anatupungia mkono. Ingieni nyie kwanza… nitazungumza na daktari kwanza..

**SFX: Sauti ya kifaa cha kusaidia maisha kinasikika**

**11.BETI**: Ni baba kweli?..(**akikaribia kulia**) amedhoofika sana…

**12.RONNIE**: Amekonda sana labda hawampi chakula

**13.BETI**: Anatusikia?..(**aita polepole**) ba.. baba..?

**14.EVELINE**: Daktari amesema anatusikia lakini ataweza kutujibu atakapopata nafuu zaidi…

**15.RONNIE**: Eve, samahani kama nitakuudhi.. lakini inawezekana kuwa baba alipigwa risasi na mpinzani wako katika siasa?

**16.EVELINE**: Sijui kakangu lakini niliripoti na kesi iko mikononi mwa polisi .. atakayekamatwa atashtakiwa kwa mujibu wa sheria…

**17: BETI**: Je naweza kumuimbia baba?

**18.EVELINE**: Eeh sawa tu muimbie dada.. lakini uimbe na sauti ya chini usitatize shughuli za hospitali..

**19.BETI**: (**aimba wimbo wa malaika polepole)**

**Mwisho wa kipindi cha nane.**

**Msimulizi:**

Na wimbo huo ukaanza kutanda anga ya chumba cha hospitali alikolazwa Mapito huku watoto wake watatu wakiwa wameketi kando ya kitanda chake. Je Mapito ataamka? Ni kitu gani kinachomsubiri Eveline katika baraza la mji baada ya kushinda udiwani? Na kuna jambo la kuwashangaza Roni na Betty! Ni lipi hilo? Ukitaka kujua msikilizaji jiunge nasi wiki ijayo. Kumbukua unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye tovuti yetu. www.dw-world.de/lbe